



ISSN 0856-6976

MUHTASARI WA TAMKO LA SERA YA FEDHA

2022/23

**GAVANA
BENKI KUU YA TANZANIA**

Juni 2022



ISSN 0856-6976

MUHTASARI WA TAMKO LA SERA YA FEDHA

2022/23

**GAVANA
BENKI KUU YA TANZANIA**

Juni 2022



UTANGULIZI

Kwa mujibu wa Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Kifungu cha 21(3) hadi (6), Sura ya 197, Benki Kuu ya Tanzania inatakiwa kutoa Tamko la Sera ya Fedha mwezi Juni kila mwaka, likifuatiwa na tathmini ya nusu mwaka mwezi Februari. Tamko la Sera ya Fedha hutoa tathmini ya matokeo ya utekelezaji wa sera ya fedha ikilinganishwa na malengo mapana ya Serikali na ya sera ya fedha. Tamko hili la Sera ya Fedha la Juni 2022, linajumuisha tathmini ya utekelezaji wa sera ya fedha ikilinganishwa na malengo kwa mwaka 2021/22, pamoja na mapitio ya mwenendo wa uchumi wa dunia na wa Tanzania. Vilevile, Tamko hili linatoa mwelekeo wa uchumi wa dunia na wa ndani na kuweka malengo ya sera ya fedha kwa mwaka 2022/23.

Utekelezaji wa Malengo ya Sera ya Fedha ya Mwaka 2021/22

Katika mwaka 2021/22, Benki Kuu iliendelea kutekeleza sera ya fedha inayolenga kuhakikisha uwepo wa ukwasi wa kutosha ili kusaidia kufufua shughuli za kiuchumi zilizoathiriwa na janga la UVIKO-19. Utekelezaji wa sera ya fedha ulikusudia kufikia malengo mapana ya Serikali ya ukuaji wa Pato la Taifa wa asilimia 5 kwa mwaka 2021 na kuhakikisha mfumuko wa bei unabaki ndani ya wigo wa kati ya asilimia 3–5. Ili kufikia malengo haya, Benki Kuu ililenga kutekeleza sera ya fedha yenye malengo yafuatayo:

- i. ukuaji wa fedha taslimu wa asilimia 9.9;
- ii. ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) wa asilimia 10;



- iii. ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi wa asilimia 10.6; na
- iv. kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayotosha kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

Katika kufikia malengo hayo, Benki Kuu ilitumia nyenzo mbalimbali za sera ya fedha ili kuhakikisha uwepo wa ukwasi wa kutosha katika uchumi. Nyenzo hizi zilijumuisha utoaji wa mikopo ya muda mfupi kwa mabanki, pamoja na kuuza na kununua fedha za kigeni katika soko la jumla la fedha za kigeni. Aidha, hatua nyingine za sera ya fedha zilitekelezwa kuanzia mwezi Julai 2021 ili kuongeza ukwasi, hivyo kuongeza chachu ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi na kuweka mazingira wezeshi kwa taasisi za fedha kupunguza riba za mikopo.

Utekelezaji wa sera ya fedha ulifanikiwa kwa kiasi kikubwa, licha ya changamoto kadhaa zilizojitokeza katika nusu ya pili ya mwaka, zilizotokana zaidi na athari za ongezeko la bei za bidhaa katika soko la dunia na kuibuka kwa aina mpya ya virusi vya UVIKO-19 katika baadhi ya nchi washirika wa kibiashara, hususan China. Changamoto hizi zilichangiwa pia na kuvurugika kwa mnyororo wa ugavi wa bidhaa na huduma katika soko la dunia na athari za vita nchini Ukraine. Hata hivyo, utekelezaji wa sera ya fedha ulisaidia kuendeleza utulivu wa riba katika masoko ya fedha na uwepo wa ukwasi wa kutosha katika mabanki. Vilevile, ukuaji wa fedha taslimu, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi na mikopo kwa sekta binafsi uliongezeka kwa kiasi kikubwa ukilinganishwa na mwaka 2020/21.



Wakati huo huo, wastani wa riba za mikopo inayotolewa na sekta ya benki ulipungua, japo kwa kasi ndogo, na kufikia asilimia 16, hali inayoashiria uwepo wa changamoto nyingine za kimfumo.

Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi ulikua kwa wastani wa asilimia 13.1 katika kipindi cha Julai 2021 hadi Aprili 2022, ikilinganishwa na lengo la ukuaji wa asilimia 10 kwa mwaka 2021/22. Ukuaji wa fedha taslimu ulifikia wastani wa asilimia 13.8, ukilinganishwa na lengo la asilimia 9.9. Aidha, ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi uliendelea kuongezeka na kufikia wastani wa asilimia 8.4, ukilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2020/21 na lengo la ukuaji wa asilimia 10.6. Mafanikio haya yamechangiwa zaidi na utekelezaji wa sera ya fedha na kuimarika kwa mazingira ya kibiashara nchini.

Thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya sarafu mbalimbali duniani imeendelea kuwa tulivu katika kipindi chote cha kuanzia Julai 2021 hadi Aprili 2022, hali iliyochangiwa kwa kiasi kikubwa na utulivu wa mfumuko wa bei nchini, utekelezaji madhubuti wa sera ya fedha na bajeti, na uwepo wa akiba ya kutosha ya fedha za kigeni. Akiba ya fedha za kigeni iliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 5,461.4 mwishoni mwa mwezi Aprili 2022, kutoka dola za Marekani milioni 4,969.7 mwezi Aprili 2021. Akiba hii inatosha kulipia uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi 5. Kiwango hiki ni sawia na lengo la nchi la kukidhi miezi isiyopungua minne na kigezo cha mtangamano wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki cha kukidhi miezi isiyopungua minne na nusu.



Mwenendo wa Uchumi wa Dunia

Uchumi wa dunia uliendelea kuimarika katika nusu ya pili ya mwaka 2021. Aidha, kasi ya kuimarika kwa uchumi wa dunia imeanza kuathirika kutokana na kuongezeka kwa bei za bidhaa katika soko la dunia, vita nchini Ukraine na kuibuka kwa aina mpya ya virusi vya UVIKO-19 nchini China. Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), linakadiria ukuaji wa uchumi wa dunia wa asilimia 6.1 mwaka 2021, nchi zilizo kusini mwa Jangwa la Sahara (SSA) (asilimia 4.5), Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) (asilimia 4.4) na asilimia 6.2 kwa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC). Aidha, IMF ilirekebisha na kupunguza makadirio ya ukuaji wa uchumi wa dunia kwa mwaka 2022 na 2023 kwa asilimia 0.8 na asilimia 0.2 ya makadirio ya awali, kufikia asilimia 3.6 kwa kipindi chote, kutokana na changamoto zinazoikumba dunia na hatua za sera za fedha katika kupunguza athari za mfumuko wa bei. Ukuaji wa uchumi kwa nchi zilizo kusini mwa Jangwa la Sahara unatarajiwa kuwa asilimia 3.8 mwaka 2022 na asilimia 4 kwa mwaka unaofuata. Ukuaji wa uchumi wa nchi za SADC unatarajiwa kufikia wastani wa asilimia 3.1 na asilimia 3 kwa mwaka 2022 na 2023, mtawalia. Katika kipindi hicho, ukuaji wa uchumi wa nchi za EAC unatarajiwa kuwa asilimia 5.3 na asilimia 5.6, mtawalia.

Mfumuko wa bei uliongezeka katika nchi nyingi duniani kutokana na mikwamo kwenye minyororo ya ugavi kutokana na athari za vita nchini Ukraine, pamoja na ongezeko la mahitaji. Katika nchi zilizoendelea, mfumuko wa bei ulikuwa juu ya malengo, hususan katika nchi za Marekani, Uingereza na Umoja wa Ulaya. Mfumuko



wa bei katika nchi za EAC umeongezeka japo umeendelea kubakia katika kiwango kilichokubalika cha chini ya asilimia 8. Mfumuko wa bei uliongezeka pia katika nchi za SADC, huku baadhi ya nchi zikiwa na mfumuko wa bei ulio juu ya kigezo cha mtangamano wa kiuchumi wa asilimia 3-7, isipokuwa kwa Tanzania, Afrika Kusini, visiwa vya Shelisheli, Eswatini na Namibia. Benki kuu nyingi duniani zimeanza kubadili uelekeo wa sera za fedha, ikiwa ni pamoja na kupunguza kasi ya kuongeza ukwasi, sambamba na hatua nyingine zinazoendelea kuchukuliwa ili kukabiliana na ongezeko la mfumuko wa bei. Kutokana na kupanda kwa kasi ya mfumuko wa bei duniani, benki kuu nyingi zimekumbwa na changamoto ya namna bora ya kukabili mfumuko wa bei bila kuathiri kasi ya ukuaji wa shughuli za kiuchumi ambazo bado hazijatengemaa kutokana na athari za janga la UVIKO-19.

Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) linatarajia mfumuko wa bei kuendelea kuwa juu katika nchi nyingi duniani kwa mwaka 2022, kufuatia kuvurugika kwa mnyororo wa ugavi uliochangia kuongezeka kwa bei za vyakula na mafuta katika soko la dunia. Mfumuko wa bei katika nchi zilizo kusini mwa Jangwa la Sahara unatarajiwa kuwa wa juu, kiasi cha asilimia 12.2 mwaka 2022, na kupungua hadi kufikia asilimia 9.6 mwaka 2023. Katika nchi za EAC na SADC, mfumuko wa bei unatarajiwa kuwa asilimia 6.2 na asilimia 9.9 mwaka 2022, na kupungua hadi asilimia 6 na asilimia 7 mwaka 2023, mtawalia.



Bei za bidhaa hususan bidhaa za petroli, mbolea na bidhaa za walaji ziliongezeka kwa kiwango kikubwa kutokana na kutokuwepo kwa uwiano wa mahitaji na ugavi, huku vita nchini Ukraine ikiongezea makali changamoto hii. Bei za mafuta ziliongezeka na kufikia zaidi ya dola za Marekani 100 kwa pipa, huku bei ya juu ikiwa ni dola za Marekani 118 kwa pipa mwezi Aprili 2022. Bei za mafuta zinatarajiwa kupungua hadi kufikia dola za Marekani 80 kwa pipa kuanzia mwezi Februari 2023 kutokana na matarajio ya kuongezeka kwa uzalishaji. Aidha, bei ya dhahabu imeendelea kuwa juu kati ya dola za Marekani 1,850-1,947.81 kwa aushi moja, japo inatarajiwa kupungua kutokana na nchi zilizoendelea kuanza kutekeleza sera ya fedha ya kupunguza ukwasi kwenye uchumi ili kupunguza mfumuko wa bei.

Mwenendo wa Uchumi wa Tanzania

Tanzania Bara

Uchumi wa Tanzania ulikua kwa asilimia 4.9 mwaka 2021, ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.8 kwa mwaka 2020. Shughuli zilizochangia ongezeko hili ni kilimo (asilimia 19.6), ujenzi (asilimia 13.1), uchimbaji madini na mawe (asilimia 8.8), uzalishaji viwandani (asilimia 8), biashara (asilimia 6.2) na usafirishaji na uhifadhi mizigo (asilimia 5.7). Aidha, shughuli zilizokua kwa kasi ya juu zaidi ni pamoja na sanaa na burudani (asilimia 19.4), umeme (asilimia 10), uchimbaji madini na mawe (asilimia 9.6), na habari na mawasiliano (asilimia 9.1).



Mfumuko wa bei nchini umeendelea kuwa tulivu ndani ya malengo ya kati ya asilimia 3-5 na vigezo vya mtangamano wa kiuchumi kikanda (EAC na SADC), licha ya kupanda kwa bei za bidhaa katika soko la dunia, hususan bidhaa za petroli, ngano na mafuta ya kupikia. Katika kipindi cha Julai 2021 hadi Aprili 2022, mfumuko wa bei ulikuwa wastani wa asilimia 3.9 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2020/21. Ongezeko hili lilitokana na kupanda kwa bei za nishati, bidhaa na huduma za chakula na zisizo za chakula. Aidha, mfumuko wa bei usiojumuisha bei za vyakula visivyochakatwa, nishati, na maji; ambao huchangia takriban asilimia 73.9 ya mizania yote katika fahirisi za bei za bidhaa, ulikuwa asilimia 3.9 ukilinganishwa na asilimia 3 katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Kwa upande mwingine, ongezeko kubwa na mfumuko wa bei likitokana na kupanda kwa bei za vifaa vya ujenzi, usafiri na kodi za majengo. Mfumuko wa bei za nishati na mafuta ulikuwa asilimia 5.5 ukilinganisha na asilimia 4.1. Mfumuko wa bei za vyakula uliongezeka kufikia wastani wa asilimia 5.1 kutoka asilimia 3.6 kutokana na ongezeko la mahitaji ya chakula kutoka kwa baadhi ya nchi jirani na kupungua kwa mavuno ya msimu wa mvua za vuli. Mfumuko wa bei usiohusisha bei za vyakula uliongezeka kidogo kufikia wastani wa asilimia 3.4 kutoka asilimia 3.1. Kutokana na ongezeko la bei za bidhaa nchini lililosababishwa na kupanda kwa bei za bidhaa mbalimbali katika soko la dunia, hususan petrol, bidhaa za chakula, na mbolea, mfumuko wa bei unatarajiwa kuongezeka. Pamoja na kuongezeka, mfumuko wa bei unatarajiwa kubaki ndani ya wigo wa asilimia 3-5 mwezi Juni 2022.



Ukuaji wa ujazi wa fedha na mikopo kwa sekta binafsi uliendelea kuongezeka sambamba na utekelezaji wa sera ya fedha inayolenga kuongeza ukwasi kwenye uchumi na sera wezeshi ya bajeti. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi ulikua kwa wastani wa asilimia 13.1 katika kipindi cha kuanzia Julai 2021 hadi Aprili 2022 ukilinganishwa na wastani wa asilimia 6.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2020/21. Wakati huohuo, wastani wa fedha taslimu ulikua kwa asilimia 13.8 ukilinganishwa na ukuaji wa asilimia 2.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2020/21. Hata hivyo, utekelezaji wa sera ya fedha ulikumbwa na changamoto za ongezeko la bei za bidhaa katika soko la dunia, hususan katika robo ya tatu ya mwaka 2021/22, hali iliyochangiwa na kuvurugika kwa mnyororo wa ugavi wa bidhaa na huduma na madhara ya vita inayoendelea nchini Ukraine. Changamoto hizi kutoka nje ya nchi, zilichangia kuongezeka kwa mfumuko wa bei nchini.

Pamoja na changamoto zilizotajwa, ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi uliendelea kuimarika sanjari na kuendelea kutengemaa kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi ikichangiwa na sera wezeshi za fedha na bajeti na jitihada zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali katika kuboresha mazingira ya kufanya biashara na kuendelea kufunguka kwa biashara duniani. Wastani wa ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi uliongezeka na kufikia asilimia 8.4 katika kipindi cha Julai 2021 hadi Aprili 2022, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2020/21 na lengo la ukuaji wa asilimia 10.6 kwa mwaka 2021/22. Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi unatarajiwa kuendelea kuimarika ukichangiwa na hatua



zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali katika kuboresha mazingira ya biashara na sera za fedha na bajeti.

Mapato ya Serikali yalikuwa ya kuridhisha katika kipindi cha Julai 2021 hadi Aprili 2022, licha ya changamoto zilizotokana na athari za UVIKO-19 na vita nchini Ukraine. Ukusanyaji wa mapato ya ndani (mapato ya kodi na yasiyo ya kodi) ulifikia shilingi bilioni 19,986.3, ambapo makusanyo ya kodi yalikuwa shilingi bilioni 16,470.7. Mikopo na misaada kutoka nje ya nchi ilikuwa shilingi bilioni 5,723.8. Serikali imeendelea kuoanisha matumizi na mapato, kipaumbele kikielekezwa katika utekelezaji wa miradi ya kimkakati na ujenzi wa miundombinu, pamoja na kugharamia shughuli za kijamii, hususan afya, maji na elimu. Jumla ya matumizi yote ya Serikali yalikuwa shilingi bilioni 26,103.2, sawa na asilimia 94.2 ya makadirio kwa kipindi husika, ambapo asilimia 51.2 yalikuwa matumizi ya kawaida. Deni la Serikali la nje na la ndani lilifikia dola za Marekani milioni 30,139.1 mwishoni mwa mwezi Aprili 2022, kutoka dola za Marekani milioni 28,011.2 mwezi Juni 2021, huku deni la Serikali la nje likiwa sawa na asilimia 67.7. Pamoja na kuongezeka, deni hili limeendelea kuwa himilivu.

Sekta ya nje imeendelea kukumbana na changamoto zinazotokana na athari za vita ya Ukraine na athari za UVIKO-19, zinazoendelea kusababisha ongezeko la bei za bidhaa na mkwamo wa ugavi duniani. Nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamishaji mali nchi za nje iliongezeka kufikia dola za Marekani milioni 2,904.2 katika kipindi cha Julai 2021 hadi Aprili 2022 kutoka



dola za Marekani milioni 1,324.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2020/21. Ongezeko hili lilitokana na kupanda kwa bei ya bidhaa na huduma zilizoagizwa kutoka nje ya nchi, hususan bidhaa za petroli. Aidha, katika kipindi cha Julai 2021 hadi Aprili 2022, urari wa malipo nje ya nchi ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 405.5, ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 141.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2020/21, kutokana na kuongezeka kwa misaada na mikopo kwa Serikali kutoka nje ya nchi.

Nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamishaji mali nchi za nje inatarajiwa kufikia asilimia 4.5 ya Pato la Taifa mwaka 2022/23. Hii inatokana zaidi na kuongezeka kwa gharama ya uagizaji bidhaa kutoka nje ya nchi kunakosababishwa na ongezeko la bei za bidhaa katika soko la dunia, hususan nishati na vyakula.

Zanzibar

Uchumi wa Zanzibar ulikua kwa asilimia 5.1 mwaka 2021 ukilinganishwa na ukuaji wa asilimia 1.3 mwaka 2020, kutokana na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi. Shughuli zilizochangia ongezeko hili ni malazi na huduma za chakula, mifugo, ujenzi, kilimo, upangishaji majengo na uzalishaji viwandani. Uchumi wa Zanzibar unatarajiwa kukua kwa asilimia 6.8 mwaka 2022 na asilimia 7.2 mwaka 2023.

Mfumuko wa bei umeendelea kuwa tulivu katika viwango vya chini, ndani ya lengo la muda wa kati la ukomo wa asilimia 5. Mfumuko wa bei wa jumla ulikuwa wastani wa asilimia 2.7 katika kipindi cha



Julai 2021 hadi Aprili 2022 kutoka asilimia 1.6 kipindi kama hicho mwaka 2020/21, kutokana na ongezeko la bei za bidhaa za petroli. Mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kubakia ndani ya lengo la tarakimu moja katika kipindi kilichosalia cha mwaka 2021/22 na mwaka unaofuata, licha ya athari zinazotokana na ongezeko la bei za bidhaa katika soko la dunia.

Aidha, mapato ya Serikali yameendelea kuongezeka kutokana na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi, hususan zile zinazohusiana na utalii na kuimarika kwa jitihada za ukusanyaji na usimamizi wa mapato. Jumla ya mapato yalifikia shilingi bilioni 790.1 katika kipindi cha Julai 2021 hadi Aprili 2022, ambapo mapato ya ndani yalikuwa shilingi bilioni 748 ikiwa ni asilimia 77.2 ya lengo, na misaada kutoka kwa wahisani wa maendeleo ikiwa ni shilingi bilioni 42.2. Mapato ya kodi yaliongezeka kwa asilimia 13.5 hadi kufikia shilingi bilioni 609.5, ikilinganishwa na kiwango kilichokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka 2020/21. Aidha, mapato yasiyo ya kodi yalikuwa shilingi bilioni 138.5, sawa na asilimia 86.9 ya lengo. Matumizi ya Serikali yaliendelea kuoanishwa na malengo, vipaumbele na mapato. Katika kipindi cha Julai 2021 hadi Aprili 2022, matumizi ya Serikali yalifikia shilingi bilioni 973.9, sawa na asilimia 88.5 ya makadirio. Matumizi ya kawaida yalikuwa shilingi bilioni 608.6, sawa na asilimia 82.8 ya makadirio, na matumizi ya maendeleo yalikuwa shilingi bilioni 365.4 ikiwa ni asilimia 99.9 ya makadirio. Deni la Serikali liliongezeka na kufikia shilingi bilioni 1,224.4 mwezi Aprili 2022, kutoka shilingi bilioni 887 mwishoni mwa mwezi Juni 2021, ambapo deni la nje lilikuwa ni asilimia 73.7.



Sekta ya nje ilikumbwa na misukosuko inayotokana na mvutano unaoendelea Ulaya Mashariki, ambao umesababisha kuvurugika kwa ugavi wa bidhaa na huduma katika soko la dunia na kusababisha ongezeko la bei. Kutokana na hali hii, nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamishaji mali nchi za nje iliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 186.1 katika kipindi cha Julai 2021 hadi Aprili 2022, ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 173.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2020/21. Ongezeko hili lilichangiwa zaidi na kuongezeka kwa gharama za uagizaji wa bidhaa za mafuta na chakula, ambazo zilikuwa kubwa ikilinganishwa na ongezeko la mapato yaliyotokana na mauzo ya karafuu na shughuli za utalii.

Sekta ya Benki

Sekta ya benki imeendelea kuwa imara na yenye kutengeneza faida, ikiwa na mtaji na ukwasi wa kutosha, hali inayoashiria uthabiti dhidi ya mitikisiko ya kiuchumi duniani. Viwango vya amana na rasilimali vimeendelea kuongezeka, ikiwa ni pamoja na kuendelea kuimarika kwa rasilimali, kufuatia kupungua kwa uwiano wa mikopo chechefu kufikia asilimia 8.2 ya mikopo yote mwezi Aprili 2022, kutoka asilimia 9.3 mwezi Juni 2021. Hali hii ilitokana na hatua zilizochukuliwa na Benki Kuu katika kupunguza uwiano wa mikopo chechefu kufikia kiwango kinachokubalika kisichozidi asilimia 5. Baadhi ya hatua hizo ni pamoja na kuzitaka benki na taasisi zote za fedha kuzingatia viashiria vya sifa za mkopaji na kusesitiza matumizi ya kanzidata ya taarifa za wakopaji katika mchakato wa kutoa



mikopo mipya. Vilevile, Benki Kuu inafuatilia na kuhakikisha kuwa benki zinatekeleza mikakati ambayo zimeainisha katika kuhakikisha mikopo chechefu inaendelea kupungua, pamoja na kuzitaka benki kuwasilisha taarifa zao za mikopo kwenye kanzidata ya taarifa za wakopaji. Aidha, Benki Kuu inaendelea kuwataka watumishi wa benki zote kuzingatia maadili ya kiutendaji ili kuongeza uadilifu wa wafanyakazi.

Masoko ya Fedha

Soko la hatifungani na dhamana za Serikali limeendelea kuimarika na kufanikisha utekelezaji wa bajeti za Serikali katika kipindi cha Julai 2021 hadi April 2022. Mwezi Novemba 2021, Serikali ilianza mpango wa kuboresha soko la hatifungani kwa kuziingiza kwenye mnada kwa mara ya pili hati fungani ambazo zilishauzwa katika minada iliyopita (*Treasury bond reopening*), ikiwa ni moja ya hatua za kuongeza ukwasi na kuboresha uchakataji mzuri wa bei (*price discovery*) katika soko la hatifungani. Vilevile, Serikali ilipitia na kupunguza viwango vya gawio kwenye hati fungani (*coupon rates*) mwezi Aprili 2022 kwa kuoanisha na viwango vya riba katika soko la fedha.

Aidha, Benki Kuu iliendelea kutoa elimu kwa umma juu ya uwekezaji kwenye hatifungani na dhamana za Serikali, jitihada ambazo zimechangia katika kuongezeka kwa wawekezaji wadogo kwenye minada ya dhamana na hatifungani za Serikali na kufikia asilimia 14.6 mwezi Mei 2022 kutoka asilimia 7.8 mwezi Julai 2021. Soko



la hatifungani na dhamana za Serikali linatarajiwa kuimarika zaidi kwa kuongezeka kwa ushindani katika siku za mbeleni kufuatia kupitishwa kwa Kanuni za Fedha za Kigeni za mwaka 2022. Kanuni hizo mpya zinaruhusu wakazi wa nchi za SADC na EAC kuwekeza katika dhamana za Serikali za muda mfupi na mrefu. Aidha, Kanuni hizo zinaruhusu mkazi wa Tanzania kuwekeza katika nchi wanachama wa jumuiya hizo. Hatua hii inatarajiwa kupanua wigo wa uwekezaji na ushindani katika kuwekeza katika hatifungani na dhamana za Serikali.

Mifumo ya Malipo

Mifumo ya malipo imeendelea kufanya kazi kwa ufanisi, ikiakisi ongezeko la matumizi ya mifumo ya kidigitali kufuatia maamuzi ya kisera ya kuongeza ukomo wa kiwango cha miamala na akiba kwenye akaunti za simu za mkononi na utumiaji wa teknolojia za kutoa huduma za kifedha kwa wafanyabiashara wadogo na wakubwa. Mafanikio makubwa yameendelea kufikiwa kupitia mifumo hii, ambapo idadi ya watu wazima waliofikiwa na huduma za fedha kupitia simu zao za mikononi ilikuwa asilimia 80.8 mwezi Machi 2022, ikilinganishwa na asilimia 78.7 kwa mwaka 2020/21. Matumizi ya simu za mikononi hapa nchini yamekuwa chachu ya kufikisha huduma za fedha kwa makundi yasiyofikiwa na huduma rasmi za kibenki. Matumizi ya huduma za fedha kupitia simu za mikononi yaliongezeka kufikia asilimia 94.3 mwezi Machi 2022, ikilinganishwa na asilimia 93.2 kwa mwaka 2020/21. Aidha, matumizi ya mifumo ya kiteknolojia kwa sekta binafsi na ya umma



yamechangia kwa kiwango kikubwa kupunguza gharama za huduma za kifedha hivyo kuchangia katika shughuli za uzalishaji.

Vilevile, Benki Kuu imeendelea na zoezi la kukamilisha uundwaji wa Mfumo wa Malipo ya Papo kwa Hapo Nchini (*Tanzania Instant Payment System*), unaolenga kurahisisha na kuboresha muingiliano baina ya mifumo mbalimbali ya watoa huduma za malipo ya fedha nchini. Mfumo huu ulianza majaribio kwa kufanya kazi na watoa huduma za fedha watano na umeendelea kuonesha kiwango kikubwa cha ongezeko la idadi na thamani ya miamala. Kukamilika kwa mfumo huu kutakuwa na faida nyingi za kiuchumi, zikiwemo kuchochea huduma jumuishi za kifedha, kupunguza matumizi ya fedha taslimu, na kuhamasisha usimamizi na kukuza matumizi ya huduma za fedha kidigitali.

Matarajio ya Uchumi na Malengo ya Sera ya Fedha ya Mwaka 2022/23

Malengo ya kiuchumi ya Serikali yamehuishwa na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22-2025/26 na Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar. Mipango hii inajikita katika kufanikisha ukuaji na maendeleo jumuishi kwa ajili ya kujenga uchumi shindani wa viwanda kwa maendeleo ya watu. Aidha, kutokana na changamoto zinazotokana na athari za UVIKO-19 na madhara yatokanayo na misukosuko ya kiuchumi duniani, malengo mapana ya kiuchumi ya Serikali kwa mwaka 2022/23 kwa Tanzania bara ni kama yafuatayo:



- i. ukuaji wa Pato halisi la Taifa wa asilimia 4.7 kwa mwaka 2022 na asilimia 5.3 kwa mwaka 2023; na
- ii. mfumuko wa bei wa kiwango cha tarakimu moja wa asilimia 5.4 kwa 2022/23.

Kwa upande wa uchumi wa Zanzibar, Serikali inalenga kufikia malengo yafuatayo:

- i. ukuaji wa Pato la Taifa wa asilimia 6.8 kwa mwaka 2022 na asilimia 7.2 kwa mwaka 2023; na
- ii. mfumuko wa bei ulio chini ya wastani wa asilimia 5 kwa mwaka 2022/23.

Sera ya Fedha ya Mwaka 2022/23

Ili kufikia malengo mapana ya Serikali ya ukuaji wa uchumi na mfumuko wa bei katika mwaka 2022/23, na kwa kuzingatia changamoto zitokanazo na ongezeko la bei za bidhaa katika soko la dunia, Benki Kuu itaendelea kuhakikisha utulivu wa mfumuko wa bei, huku ikiendelea kutekeleza sera ya fedha inayolenga kuongeza ukwasi ili kulinda ukuaji wa uchumi nchini. Aidha, Benki Kuu itaendelea kufuatilia kwa karibu zaidi mwenendo wa mfumuko wa bei nchini, na inaweza kuanza kupunguza kasi ya ongezeko la ukwasi kwenye uchumi, pindi itakapohitajika. Ili kufikia malengo mapana ya Serikali kwa mwaka 2022/23, Benki Kuu ya Tanzania imepanga kutekeleza sera ya fedha yenye malengo yafuatayo:



- i. ukuaji wa fedha taslimu wa asilimia 11.4;
- ii. ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) wa asilimia 10.3;
- iii. ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi wa asilimia 10.7; na
- iv. kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayotosha kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

Vilevile, Benki Kuu itaendelea kuchukua hatua kadhaa kwa lengo la kuboresha mfumo wa kutekeleza sera ya fedha kuelekea matumizi ya riba kama kiashiria cha sera ya fedha. Hatua hizi ni pamoja na kuboresha mfumo wa modeli za kiuchumi zitakazokuwa zikitumika kufanya uchambuzi wa kisera, kuendelea kutoa elimu kwa wadau wote juu ya mfumo huu, kuandaa mwongozo wa utekelezaji wa sera ya fedha kwa kutumia riba ya Benki Kuu ya Tanzania na kuendelea kufanya maboresho katika sekta ya fedha kwa lengo la kuongeza ufanisi.



Hitimisho

Ukuaji wa uchumi katika mwaka 2021 ulikuwa wa kuridhisha na kasi ya mfumuko wa bei ilikuwa ndani ya lengo kwa mwaka 2021/22, licha ya kukabiliwa na changamoto za madhara ya kuibuka kwa aina mpya ya virusi vya UVIKO-19 na vita nchini Ukraine. Changamoto hizi zinatarajiwa kuendelea katika nusu ya kwanza ya 2022/23, na kuanza kupungua katika nusu ya pili. Kutokana na hali hiyo, uchumi wa Tanzania Bara unatarajiwa kukua kwa asilimia 4.7 mwaka 2022, na asilimia 6.8 kwa Zanzibar. Ukuaji huu wa uchumi utachangiwa kwa kiasi kikubwa na shughuli za uwekezaji zinazoendelea kufanywa na Serikali, kuendelea kuimarika kwa shughuli za sekta binafsi na uchumi wa dunia, pamoja na utekelezaji wa mipango ya maendeleo katika kuboresha uchumi wa buluu na kuimarika kwa shughuli za utalii.

Mfumuko wa bei kwa Tanzania Bara na Zanzibar ulikuwa ndani ya malengo kwa mwaka 2021/22, aidha unatarajiwa kuongezeka kidogo mwaka 2022/23 kutokana na changamoto zilizopelekea kupanda kwa bei za bidhaa katika soko la dunia. Hata hivyo, kasi ya mfumuko wa bei inatarajiwa kuendelea kubakia ndani ya malengo ya nchi na viwango vinavyokubalika kikanda. Kwa msingi huu, Benki Kuu ya Tanzania itaendelea kutekeleza sera ya fedha inayolenga kuweka mazingira wezeshi ya kulinda ukuaji wa uchumi, bila kuathiri lengo la kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei. Katika kufikia malengo haya, Benki Kuu ya Tanzania itaendelea kutumia kwa makini nyenzo mbalimbali za usimamizi na utekelezaji wa sera ya fedha kwa uthabiti na umakini mkubwa.



Aidha, Benki Kuu ya Tanzania itaendelea kutekeleza hatu ambalimbali za kuboresha mfumo wa utekelezaji wa sera ya fedha unaotumia riba kama kiashiria cha ukwasi kwenye uchumi, ili kuongeza ufanisi wa sera ya fedha katika kusimamia mfumuko wa bei na kuchochea ukuaji wa uchumi. Vilevile, Benki Kuu kwa kushirikiana na wadau wengine itaendelea kufanya maboresho ya kimfumo na usimamizi wa sekta ya fedha, kwa lengo la kuongeza ufanisi. Kwa muktadha huo, ni matarajio ya Benki Kuu kuwa malengo ya sera ya fedha yaliyowekwa katika Tamko hili la Sera ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2022/23 yatafikiwa.

Kwa maelezo zaidi tafadhali wasiliana na:
Mkurugenzi wa Utafiti na Sera za Uchumi
Benki Kuu ya Tanzania, 16 Barabara ya Jakaya Kikwete 40184, S. L. P 2302,
Dodoma, Tanzania
Barua pepe: botcommunications@bot.go.tz
Tovuti: <https://www.bot.go.tz>